

# VITABU VYA MANABII

## Kitabu 1

*Mafundisho juu ya  
ISAYA*

Mwandishi : ELEZOHAKI

**Everyday Publications Inc**  
310 Killaly St. West  
Port Colborne, ON  
Canada L3K 6A6

ISBN 978-0-88873-184-5

*Imprimé au Canada*

copyright © 1972 William MacDonald All Rights Reserved

## **SOMA MANENO HAYA**

Mungu aliita watu wengi kuhubiri habari zake. Manabii kumi na sita waliandika unabii wao wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Utakuta maneno waliyoandika ndani ya Biblia.

Sehemu nyingine za vitabu vya Manabii ni nguvu kufahamu lakini kuna mafundisho mengi ya faida kwa roho zetu kutuonyeshea utakatifu na mapendo ya Mungu, na kutuonya na kutufariji. Hivi ni sharti kwetu kuvisoma.

Siku nyingine utakutana na Isaya na Yeremia na manabii hawa wote mbinguni. Utapata haya mbele yao kama hujui maneno waliyoandika ndani ya vitabu vyao!

Kitabu hiki ni kitabu cha kwanza cha vitabu vitano vya mafundisho juu ya vitabu vya Manabii:

Kitabu 1 - Isaya

Kitabu 2 - Yeremia na Maombolezo

Kitabu 3 - Ezekieli na Danieli

Kitabu 4 - Hosea kufika Nahumu

Kitabu 5 - Habakuki kufika Malaki

Soma sura moja ya Isaya kila siku pamoja na kitabu hiki kwani si faida kusoma kitabu hiki peke yake. Sharti ukisome pamoja na Biblia. Ni lazima vilevile kusoma ndani ya Biblia yako mashairi yote mengine kitabu hiki kinayotaja.

Kuna ulizo kwa mwisho wa sura nyingine. Jaribu kujibu maulizo haya, kisha angalia kwa kurasa 45 na 46 kuona kama ulijibu vizuri.

## **Vitabu vya Manabii**

Vitabu 17 vya mwisho vya Agano la Kale, ndivyo Isaya kufika Malaki, viliandikwa na manabii.

Katika Biblia nabii ndiye mtu anayesema kwa ajili ya Mungu. Mungu aliita watu wengine kuwa manabii yake wakati watu wake Waisraeli walipokwisha kuingia ndani ya zambi na kwenda mbali naye. Manabii waliwaambia watu ya kwamba walikuwa wamekosea Mungu na ya kwamba atawahukumu kama wasipotubu na kurudi kwake.

Muda wa manabii ulianza na Samweli wakati makuhani wasipotimiza mapenzi ya Mungu. Uliendelea kufika wakati Waisraeli walipotoka Babeli pahali walipokuwa wafungwa, na kurudia inchi yao na kujenga hekalu tena kwa Yerusa-lema.

Wengine wa manabii wa Agano la Kale hawakuandika vitabu vya Biblia, lakini walisema Neno la Mungu kwa kinywa.

Nyuma ya kufa kwa Mfalme Solomono ufalme ultengwa kwa sehemu mbili. Sehemu moja iliitwa Israeli na ya pili Yuda.

Nyuma yake Roho Mtakatifu aliongoza wengine wa manabii kuandika sehemu ya mafundisho yao. Nini ilitokea katika Israeli na Yuda kwa wakati wa manabii hawa? Unaweza kusoma historia ya Israeli na Yuda ndani ya vitabu vya 1 na 2 Wafalme, 1 na 2 Mambo, Ezra na Nehemiah. Ona vilevile kurasa 7-11 za kitabu hiki.

Manabii walikuwa na kazi mbili: 1) Mara nyingine ilikuwa kazi yao kusema na watu *kwa ajili ya Mungu*, maana yake

## VITABU VYA MANABII

kufundisha Neno lake kwa watu. Walifahamu vizuri neno walilokuwa wakilifanya. Tunasoma tena na tena, "Bwana alisema," au "Neno la Bwana lilifika kwangu." Kwa mfano soma Yeremia 1:9; Ezekiel 2:7.

2) Kazi ya pili ya manabii ilikuwa kutazamia wakati wa kuja na kujulisha watu nini itawapata kama wakitii Mungu au kama wakimwasi. Mara nyine manabii hawakufahamu wao wenyewe maneno walijotabiri juu ya wakati wa kuja. Kwa mfano, soma Danieli 7:28; 8:15-16, 26-27; 10:7-15. Hata mtume Yoane hakufahamu maneno yote aliyoona katika maono (Ufunuo 7:13-14; 17:6). Ilikuwa hata nguvu kupita kwa waandishi wa Agano la Kale kufahamu unabii wao juu ya Masiya atakayekuja. Walitabiri ya kwamba Kristo atateswa, na ya kwamba atakuwa na utukufu mkubwa vilevile (1 Petro 1:10-13). Iliwashinda kufahamu namna gani Masiya atateswa kama mtumishi wa Bwana, na kutawala vilevile kama Mfalme juu ya dunia nzima. Hawakufahamu ya kwamba Kristo atakuja mara mbili. Mara ya kwanza alifika kwa Betelehemu, na nyuma ya muda mrefu atakuja tena kwa Mlima wa Mizeituni.

### **Mafundisho makubwa ya manabii ya Agano la Kale yalikuwa nini?**

Manabii walihubiri maneno makubwa kumi:

1. Mungu ni mtakatifu.
2. Watu ambao Mungu aliwachagua kuwa watu wake waliingia ndani ya zambi na hawakutimiza mapenzi yake.
3. Manabii waliwaita kurudi karibu na Mungu.
4. Mungu atawahukumu kama wasipotubu.
5. Mungu atahukumu mataifa waliozunguka Israeli.
6. Wengine wa Wayuda watarudia inchi yao nyuma ya kushi miaka mingi kama watumwa katika Babeli.

## VITABU VYA MANABII

7. Masiya atakuja, lakini Wayuda watamkataa.
8. Masiya atakuja tena na uwezo na utukufu mkubwa.
9. Watu wachaguliwa wa Mungu, ndio Wayuda, watarudi karibu naye.
10. Kristo atatawala kama Mfalme juu ya dunia nzima.

Vizuri tufahamu ya kwamba manabii wa Agano la Kale hawakufundisha juu ya Kanisa. Hatuwezi kushangaa juu ya neno hili kwani Waefeso 3:4-6 yanatufundisha ya kwamba kweli ya Kanisa ilikuwa siri ambayo Mungu aliifichia watu kufika wakati wa Agano Jipy (Waefeso 3:4-6).

Mashairi mengi ndani ya Agano la Kale yana maana mbili. Kwa kuyafahamu vizuri inatupasa kukumbuka ya kwamba unabii katika mashairi mengine ulitimizwa muda mfupi tu nyuma ya wakati nabii alipoutoa au kuandika. Mara nyingine sehemu tu ya unabii ulitimizwa na tunafahamu sasa ya kwamba ulitimizwa mzima miaka mingi nyuma ya mauti ya nabii mwenyewe. Mengi ya maneno manabii wali-yotabiri hayajatimizwa bado hata sasa, lakini yatatimizwa kwa wakati wa kuja saa Bwana Yesu atakaporudi.

Kwa mfano, Yoeli aliandika ahadi ya Mungu kutuma Roho Mtakatifu juu ya watu wote walio hai (Yoeli 2:28-32). Ahadi hii ilitimizwa kwa sehemu siku ya Pentekote, lakini watu wachache tu wa wale waliokuwa hai kwa wakati ule walipokea Roho Mtakatifu (Matendo 2:16-21). Wakati Bwana Yesu atakaporudi ataanza kutawala juu ya dunia nzima na unabii wa Yoeli utatimizwa kabisa kabisa.

Tunataka kutaja maneno machache mengine ambayo yatasaidia kufahamu vitabu vya manabii:

1) Wakati manabii walipoandika juu ya **Israeli**, mara nyin-gi maneno yao yalikuwa juu ya Ufalme wa Kaskazini, ndio makabila kumi ambao walijitenga na makabila ya Yuda na Benyamina kwa wakati wa Mfalme Rehoboamu. Hata hivi mara moja moja yalikuwa juu ya taifa zima la Israeli, ndio wazao wote wa Yakobo.

## VITABU VYA MANABII

2) Wakati walipoandika juu ya **Yuda**, waliwaza karibu kila mara juu ya Ufalme wa Kusini, ndiyo makabila ya Yuda na Benjamina.

3) Jina hili **Efuraimu** lilitumiwa zaidi na Hosea wakati alipoandika juu ya Ufalme wa Kaskazini, ndiyo makabila kumi, na mara nyingine ufalme huu uliitwa nyumba ya Yosefu.

4) **Samaria** ulikuwa mji mkubwa wa Ufalme wa Kaskazini, na manabii waliutaja tena na tena.

5) **Yerusalem** ulikuwa mji mkubwa wa Ufalme wa Kusini.

6) **Ninawe** ulikuwa mji mkubwa wa Asuria.

7) Mji wa **Babeli** ulikuwa mji mkubwa wa taifa la Babeli.

8) **Damasiki** ulikuwa mji mkubwa wa Suria, inchi ndogo kwa upande wa kaskazini wa Israeli.

Manabii waliwaambia watu mara nyingi ya kwamba Mungu anachukia maneno ya kuabudu sanamu. Waisraeli wengi waliabudu sanamu juu ya vilima au mashambani, au chini ya miti.

Mungu anachukia vilevile maneno yote yasiyo haki. Manabii waliagiza wanaume wa Israeli kuhukumu maneno yote kwa haki na kutendea watu masikini mema.

Zaidi ya Waisraeli walikuwa wamefanya zambi mbaya sana, lakini wachache walibaki waaminifu kwa Bwana na walikaa kumfuata. Watu hawa wanaitwa baki la Israeli. Sehemu ndogo tu ya taifa zima walirudia inchi yao toka Babeli, ndiyo baki. Manabii walisema ya kwamba kutakuwa na baki la Israeli kwa siku za mwisho ambao wataamini Bwana (Isaya 10:22,23).

Manabii 16 waliandika unabii ndani ya Biblia yetu. Wengine waliishi wakati Waisraeli walipopelekwa kwa Babeli kama wafungwa. Wengine walisema na Waisraeli wakati

## VITABU VYA MANABII

walipokuwa wafungwa katika Babeli. Wengine wali rudi pamoja na baki la Israeli kwa inchi yao. Manabii hawa walisema na watu kujenga tena mji wa Yerusalem na hekalu na kuachana na zambi zao.

Zaidi ya manabii walitabiri kwa watu wa Yuda, lakini manabii wane walisema zaidi kwa Israeli. Wawili wa manabii walitabiri kwa watu wa Mataifa.

### **Manabii gani walisema na**

Israeli	Yuda	Mataifa
Hosea	Isaya	Nahumu
Amosi	Yeremia	Obadia
Mika	Yoeli	
Yona	Habakuki	
	Zefania	
	Ezekieli	
	Danieli	
	Hagai	
	Zekaria	
	Malaki	

### **Manabii waliishi kwa wakati gani?**

Mbele ya kwenda Babeli	Katika Babeli	Nyuma ya kurudi toka Babeli
Isaya	Ezekieli	Hagai
Yeremia	Danieli	Zekaria
Hosea		Malaki
Yoeli		
Amosi		
Obadia		
Yona		
Mika		
Nahumu		
Habakuki		
Zefania		

## VITABU VYA MANABII

Wengine wa manabii hawa walitoa habari toka Mungu kwa mataifa mawili au zaidi. Kwa mfano, Yona alikuwa nabii kwa watu wa Ninawe vilevile. Mika alitabiri kwa watu wa Yuda na kwa watu wa Israeli vilevile. Nahumu alisema na Yuda (1:15) na Ninawe vilevile. Habakuki alitabiri maneno mengi juu ya mataifa mengine.

Sharti tujue historia ya Israeli na Yuda kama tukitaka kufahamu manabii waliyoandika.

Wakati Mfalme Solomono alipokufa makabila kumi ya kaskazini ya Israeli walijitenga na Yuda na Benyamina. Nyuma yake watu wa Suria walikuwa adui wakubwa zaidi wa Israeli.

Halafu uwezo wa taifa la Asuria ulizidi kuongezeka na polepole Waasuria walishinda Ufalme mzima wa Kaskazini, ndio Israeli:

1. Mfalme Yehu alilipa kodi kwa Salmaneseri, mfalme wa Asuria katika mwaka 842 B.C. (Maana ya B.C. ni 'mbele ya kuzaliwa kwa Kristo.')
2. Mfalme Menahemu alilipa kodi kwa Tigilati-Pileseri, mfalme wa Asuria, lakini Tigilati-Pileseri alianza kuondosha wengine wa Waisraeli toka inchi yao.
3. Wakati Peka alipokuwa mfalme wa Israeli, Tigilati-Pileseri alikamata miji ya Natufati na kupeleka watu ndani yao kwa Asuria (2 Wafalme 15:29). Alishinda watu wote waliokaa kwa upande wa mashariki wa mto Yorodani na kupeleka makabila ya Rubeni na Efuraimu na nusu ya kabilia la Manase kwa inchi yake kwa mwaka 740 B.C. (1 Mambo 5:26). Tunafikili alisaidia watu wale walioua Peka, mfalme wa Israeli, na alifanyiza Hoshea mfalme kwa pahali pake.
4. Hoshea alitumikia Salmaneseri, mfalme wa Asuria, na kuli-pa kodi, lakini nyuma ya wakati alijaribu kumwasi. Alituma zawadi kwa mfalme wa Misri na alijaribu kufungana na Misri ili asiwe chini ya amri ya mfalme wa Asuria tena (2 Wafalme 17:3,4).

## VITABU VYA MANABII

5. Salmaneseri na majeshi yake walizunguka Samaria na kukamata mji huu mwaka Sargoni alipoanza kutawala kama mfalme, 722 B.C. Waasuria walipeleka Waisraeli wengi kwa inchi yao wenyewe kama wafungwa (2 Wafalme 17:5,6,18), na walilazimisha watu waliobaki inchini kulipa mali nyingi kama kodi.

Watu wa Mungu, ndio Israeli, walianza kulipa kodi kwa mfalme wa inchi ya Mataifa miaka 842 mbele ya kuzaliwa kwa Kristo. Kwa karibu miaka ile yote Waisraeli walitawaliwa na mataifa mengine. Halafu Kristo alikuja lakini watu wa Israeli walikataa kumpokea, na hata leo Israeli si taifa lenye uwezo mkubwa. Wakati Kristo atakapokuja tena, taifa la Israeli litajulikana kupita mataifa yote mengine.

### YUDA [Makabila ya Kusini]

Watu wa Asuria walishinda makabila kumi ya kaskazini, kisha walitaka kupigana na Ufalme wa Kusini vilevile. Watu wa Yuda waliogopa na Mungu aliwaambia ya kwamba Waasuria watakuja kupigana nao, lakini ya kwamba atawa-haribu. Saniharibu, mfalme wa Asuria, alifika kukamata Yerusalem wakati Hezekia alipokuwa mfalme, lakini majeshi yake yaliharibiwa (2 Wafalme 19:35).

Kisha taifa la Babeli lilizidi kupata nguvu na lilianza kupigana na Yuda. Haya ndiyo maneno yaliyotokea:

1. Yoyakimu alianza kutawala Yuda kama mfalme lakini ilimpasa kutii mfalme wa Misri.
2. Wababeli walishinda Misri na Asuria, na kwa sababu hii walipata njia kutawala Yuda vilevile kwa mwaka 606 B.C.
3. Wakati Yoyakimu alipokuwa ametawala kwa miaka mitatu au mine, Nebukadneza, mfalme wa Babeli, alifikia Yerusalem na kukamata mji wenyewe, 606 B.C. Alikamata

## VITABU VYA MANABII

nusu ya zahabu toka hekalu na kulazimisha jamaa ya mfalme kwenda Babeli kama wafungwa. Mfalme Yoyakimu na Danieli, nabii, walifungwa saa yenyewe (2 Wafalme 24:1-6; 2 Mambo 36:5-8; Danieli 1:1-6).

4. Nyuma ya miaka tisa mingine, kwa mwaka 597 B.C. Nebukadneza alipeleka Yoyakinu (aliyeitwa Yekonia au Konia vilevile) na watu wengi wengine kwa Babeli (2 Wafalme 24:10-16). Nabii Ezekieli alipelekwa Babeli kwa wakati ule.
5. Nyuma ya miaka kumi na mmoja mingine Nebukadneza alifika tena, kwa mwaka 586 B.C. Mara hii aliteketeza hekalu, aliharibu Yerusalem, na alipeleka zaidi ya watu kwa Babeli. Watu waliokuwa masikini zaidi walibaki inchini (2 Wafalme 25:2-21).
6. Watu waliobaki inchini walitawaliwa na mtawala jina lake Gedalia. Yeremia alikuwa mmoja wa watu hawa waliobaki inchini. Gedalia aliuawa, na watu wengi walikimbia kwa Misri, wakapeleka Yeremia pamoja nao (2 Wafalme 25:22-26). Watu wa Yuda walikuwa wafungwa katika Babeli kwa miaka makumi saba.

Wababeli walitawala inchi zote kwa upande ule wa dunia kufika 538 B.C. Kisha Kiro, mfalme wa Wapersia alikamata Babeli. Kiro aliruhusu Wayuda kurudia inchi yao wenyewe. Wayuda wengi walirudi pamoja na Zerubabeli kwa mwaka 537 B.C., na wengine pamoja na Ezra kwa 458 B.C.

Wapersi na Wamedi walikuwa rafiki, na Dario, Mmedi, alikuwa mfalme toka 538 B.C. kufika 536 B.C. Wamedi na Wapersi walitawala inchi hizi zote kufika 333 B.C. Kisha Wayunani walipata uwezo zaidi; mfalme wao alikuwa Alesanduro Mkubwa.

Yeremia alitabiri ya kwamba watu wa Yuda watakuwa wafungwa katika Babeli kwa miaka 70 (Yeremia 25:11; Danieli 9:2). Tunaweza kuwaza juu ya muda huu wa miaka 70 kwa njia tatu:

## VITABU VYA MANABII

1. Toka 606 B.C. (wakati Mfalme Yoyakimu alipopelekwa Babeli) kufika 536 B.C. wakati Kiro alipotoa amri kuruhusu Wayuda kurudia inchi yao.
2. Toka 590 B.C. (wakati Nebukadneza alipozunguka Yerusalem kwa kuukamata) kufika 520 B.C. wakati Wayuda walipoanza kujenga hekalu tena.
3. Toka 586 B.C. (wakati Nebukadneza alipokamata Yerusalem) kufika 516 B.C. wakati Wayuda walipomaliza kazi ya kujenga hekalu tena.

*Mwenye zambi anaweza kujua namna gani ya kwamba zambi zake zimekuwa nyeupe kama theluji?*

## WAFALME NA MANABII WALIOISHI

### KWA MUDA MMOJA

Wafalme wa Israeli	Manabii	Wafalme wa Yuda	Manabii
Yeroboamu	Yona	Yoasi, Amazia	Yoeli
	Hosea 1:1	Uzia	Isaya 1:1
	Amosi 1:1		
Peka	Mika 1:1	Yotamu	Isaya
Hoshea	Mika	Ahazi	Isaya
		Hezekia	
		Manase	
		Yosia	Yeremia
			Habakuki
			Zefania
	Yoahasi, Yoyakimu		Yeremia
	Yoyakinu	Zedekia	Yeremia

## ISAYA

Isaya, mwana wa Amozi, aliandika kitabu cha kwanza cha manabii. Maana ya **Isaya ni wokovu unatoka kwa Bwana**, na nabii huyu anatufundisha juu ya wokovu wa Mungu kupita manabii wote wengine.

Isaya aliishi kwa wakati Uzia, Yotamu, Ahazi na Hezekia walipokuwa wafalme wa Yuda. Manabii Amosi na Hosea waliishi muda mfupi mbele ya Isaya, na Mika alikuwa hai kwa wakati wa Isaya.

Isaya alitabiri ya kwamba Masiya atakuja, na Roho Mtakatifu alimwonyeshea maneno mengi yaliyotokea wakati Bwana alipokuwa duniani. Neno hili linahakikisha ya kwamba Isaya alikuwa nabii wa kweli wa Mungu, lakini watu wengi hawataki kukubali neno hili. Wanasema watu wawili au watatu waliandika kitabu hiki kinachoitwa Isaya. Wengine wanasema mtu mmoja aliandika sura 1-39; na mwingine aliandika sura 40-66. Wengine wanasema kulikuwa na wandalishi watatu: mmoja aliandika sura 1-39; mwingine sura 40-55, na wa tatu sura 56-66.

Agano Jipyä linaonyesha wazi ya kwamba mawazo haya si kweli. Bwana Yesu alitaja Isaya 6:9 na alisema shairi hili liliandikwa na Isaya (Matayo 13:14). Katika Matayo 15:7-9 alitaja Isaya 29:13 na alisema wazi ya kwamba yalikuwa masemo ya Isaya. Bwana Yesu alitaja Isaya 42:1 vilevile na kusema shairi hili liliandikwa na Isaya.

Kitabu cha Isaya kina sehemu mbili, sura 1-39, na sura 40-66. Kuna vitabu 66 ndani ya Biblia, 39 katika Agano la Kale na 27 ndani ya Agano Jipyä. Sehemu ya pili ya Isaya inatufundisha ya kwamba Masiya atateswa na kufa, na vitabu 27

## ISAYA

vya Agano Jipyä vinatufundisha maneno mengi zaidi juu ya neno hili.

Zaidi ya unabii wa Isaya ulikuwa kwa Wayuda, lakini alisema maneno mengi vilevile juu ya mataifa waliozunguka Yuda. Na alitabiri ya kwamba siku nyingine taifa zima la Israeli watarudi kwa Bwana.

### TUNAWEZA KUGAWA UNABII WA ISAYA HIVI:

Hukumu ya Mungu juu ya Yuda na Yerusalem	sura 1-12
Hukumu ya Mungu juu ya mataifa mengine	sura 13-24
Bwana atawabariki wale ambao wanamwamini	sura 25-27
Ni upumbavu kutegemea mataifa mengine	sura 28-35
Historia ya Mfalme Hezekia	sura 36-39
Haifai kwa watu wa Mungu kuabudu sanamu	sura 40-48
Waisraeli watakataa Masiya wao	sura 49-53
Bwana aliita watu kutubu, na aliahidi kuwapokea tena	sura 54-59
Kwa siku ya Bwana, Mungu atahukumu na kubariki watu wake	sura 60-66

### SURA 1

Bwana aliita watu wote mbinguni na duniani kuja kwa baraza pahali Mungu alipokuwa Mwamuzi, na Yuda na Yerusalem waliposambishwa. Kwanza Mungu alisema ya kwamba watu wa Yuda walikuwa wamemkosea (mash. 1-4). Alisema alikuwa amewaaazibu lakini hata hivi hawakurudi karibu naye (mash. 5-9). Walitoa sadaka, lakini Mungu alikataa kuzipokea isipokuwa walitii maagizo yake (mash. 10-15). Aliwaita tena kurudi karibu naye (mash. 16-20), na kuwakumbusha ya kwamba walimwamini zamani lakini sasa hawakumwamini tena (mash. 21-23). Aliwaonya waziwazi ya kwamba atawahukumu, lakini aliahidi vilevile kuwarudisha karibu naye (mash. 24-31). Neno hili litatokea wakati Bwana Yesu atakapokuja tena.

### SURA 1-3

Ndani ya shairi 13 Bwana alikataza watu wa Yuda kufika na sadaka zao kama wasipokuwa tayari kuji-toa wenyewe kwa Mungu. Mungu hataki sisi kukwamana na desturi za dini kama tusipompenda kweli kweli.

*Mwenye zambi anaweza kujua namna gani ya kwamba zambi zake zimekuwa nyeupe kama thelaji?*

### SURA 2

Nabii alisema juu ya utukufu wa Bwana Yesu Kristo wakati atakapotawala juu ya dunia (mash. 1-5). Halafu Mungu aliagiza watu wa Yuda kuacha kufika karibu na wachawi na kutegemea mali yao wenyewe na kuabudu sanamu (mash. 6-8). Kama wasipoacha maneno haya, siku kubwa na ya kuogofya ya Bwana itawapata (mash. 10-22). Mungu atanyenyekeza wenyе kiburi (mash. 11-17) na kuondosha sanamu zote (sh.18). Watu waovu watafichama ndani ya mapango (sh.19), na kutupa sanamu zao (mash. 20,21).

Sharti tutegemee Bwana tu. Watu wote watakufa, lakini Bwana ni hai milele (Zaburi 18:46).

*Kwa sababu gani ni upumbavu kwa sisi kutegemea watu?*

### SURA 3

Mungu alijulisha watu wa Yuda na Yerusalem ya kwamba kutakuwa na wakati wa njaa kali sana na ya kwamba ataondoa viongozi wao (mash. 1-8). Ndani ya shairi 9 Isaya alitoa ole ya kwanza ya ole nane; alisema na watu ya kuwa wata-pata matata kwa sababu ya zambi zao. Ole mbili za kwanza ni ndani ya sura hii, na ole sita nyingine katika sura 5.

1. **Ole** kwao wanaofanya zambi waziwazi bila kuogopa Mungu (sh.9).

## ISAYA

2. **Ole** kwa watu waovu wote (sh.4). Watawala wa Yuda hawakuwaongoza vizuri (mash. 12-15). Wanawake walikuwa wenye kiburi; kwa njia ya mavazi ambayo walivaa na kwa namna walivyotembea walikokota macho ya wanaume juu yao (sh.16). Bwana atawahukumu kwa njia ya kundosha mavazi yao mazuri yote na mapambo yao yote (mash. 17-24). Waume wao watauawa vitani (mash. 25,26).

*Tunasoma juu ya ole ngapi ndani ya sura 3?*

## SURA 4

Kwa siku ya Bwana zaidi ya wanaume watauawa, sehemu sita za saba (sh.1). Bwana atapata utukufu mkubwa (sh.2); Waisraeli watabarikiwa (mash. 3,4), na Bwana atabariki watu wote walio hai (mash. 5,6).

## SURA 5

Watu wa Yuda walifanana na mzabibu usiozaa matunda (mash. 1-7). Mungu alipanda taifa hili namna mlimaji shamba anavyopanda mzabibu. Alifanya maneno yote yaliyohitajiwa ili mzabibu huu uweze kuzaa matunda, lakini ulizaa zabibu za mwitu tu, si zabibu nzuri.

Halafu Isaya alitaja ole sita nyingine (ona 3:9-11).

3. **Ole** kwa watajiri waliokuwa na mashamba lakini walio-taka kupata zaidi (mash. 8-10).

4. **Ole** kwa wale wanaolewa (mash. 11,12).

5. **Ole** kwa wenye zambi wasioogopa Mungu (mash. 18,19).

6. **Ole** kwa watu wale wanaosema uzuri na ubaya ni sawasawa (sh.20).

7. **Ole** kwa watu wale wanaofikili wao ni wenye haki (sh.21).

8. **Ole** kwa waamuzi wanaolewa na wasiohukumu wate-

## SURA 3 – 7

nda mabaya kwa sababu watu hawa wanawapa waamuzi mali (mash. 22,23).

Mungu atahukumu watu hawa (mash. 24,25). Ataita mataifa toka mbali kutendea Israeli namna anavyotaka kwa kuwahukumu (mash. 26-30).

*Waamuzi hawakuhukumu wenyewe kosa kwa sababu gani?*

## SURA 6

Isaya aliona ono la ajabu la utukufu wa Bwana (mash. 1-4). Halafu alifahamu ya kwamba ye ye mwenyewe alikuwa mwenye zambi kabisa, na alikiri neno hili mbele ya Mungu (sh.5). Mmoja wa malaika alileta kala la moto kusafisha midomo yake (mash. 6,7). Halafu alikuwa tayari kusikia mwito wa Mungu, na Bwana alimtuma kuhubiri kwa watu wa kabilalake mwenyewe (mash. 8,9). Mungu hakuagiza Isaya kutangaza habari zitiakazofurahisha watu. Alisema ya kwamba bila shaka atahukumu taifa la Yuda, lakini ya kwamba ataachilia wengine katikati yao (mash. 10-13). Nabii aliuliza Bwana kama hukumu hii itaendelea kwa muda gani na Bwana alijibu itaendelea kufika wakati vitu vyote vitakapokwisha kuharibiwa.

Wakati ninaposoma Biblia ninajifunza ya kwamba Mungu ni mtakatifu sana. Neno hili linanisaidia kufahamu ya kwamba mimi ni mwenye zambi, na ya kwamba Mungu tu anaweza kunisafisha. Wakati moyo na midomo yangu ni safi, ninaweza kwenda kutumikia Mungu kama Isaya alivyofanya.

*Kwa nini Isaya alisema midomo yake haikuwa safi?*

## SURA 7

Roho Mtakatifu alisema na Ahazi, mfalme wa Yuda, kutegemea Mungu kumwokoa kwa pahali pa kuomba Waasuria kumlinda asishindwe na Wasuria na Waisraeli (mash. 1-9). Halafu Bwana alimpa Ahazi alama kumsaidia

## ISAYA

kuamini ya kwamba Mungu atamwokoa (mash. 10-16). Mtoto atazaliwa na kupata nguvu na kujifunza maneno mengi. Mfalme wa Suria na mfalme wa Israeli watakuwa wakati mtoto huyu asipojifunza bado mambo gani yaliyo mema na mambo gani yaliyo mabaya. Alama hii ilitimizwa miaka michache nyuma, lakini Roho Mtakatifu alikuwa akitazamia wakati wa kuja saa Bwana Yesu alipozaliwa na bikira Maria (Matayo 1:23). Halafu Bwana alimwambia mfalme wa Yuda waziwazi ya kwamba ataleta majeshi ya Misri na Asuria nao wataharibu inchi na watu wa Yuda (mash. 17-25).

*Mungu alitimiza ahadi yake katika shairi 14 wakati gani?*

## SURA 8

Isaya aliita jina la mwana wake Maheri-Salali-Hasi-Bazu, maana yake *fanya mbio kupata hazina, fanya haraka kupata wafungwa*. Alitumia jina hili kutabiri ya kwamba Waasuria watakuja mbio na kuharibu Israeli na Suria (mash. 1-4). Majeshi ya Asuria watakuja kupigana na Yuda vilevile (mash. 5-8). Adui wa Yuda watafungana pamoja, lakini Mungu atawaharibu (mash. 9,10). Haifai wale walioamini Bwana wategemee watu wengine, lakini Mungu tu. Waonyeshe neno hili kwa njia ya kushika Neno lake (mash. 11-18). Ingepasa watu kuamini Bwana; haifai wafike karibu na wenyewe ulozi na wafumu kupata kusaidia (mash. 19-22).

Kuna wafumu wengi duniani sasa wanaotaka watu kuwaamini. Watu wengine wanasema wao ni Wakristo, lakini wanataka kufundisha maneno yasiyopatana na Neno la Mungu. Tunaweza kusema na watu hawa wote: "Tutaamini maneno yale yaliyo ndani ya Biblia tu. Wewe unafundisha maneno mengine, maneno yasiyo kweli ya Mungu" (sh.20).

*Isaya na watoto wake walikuwa alama katika Israeli (sh.18). Maheri-Salali-Hasi-Bazu alikuwa alama namna gani?*

## SURA 7-10

### SURA 9

Mungu aliahidi tena ya kwamba Masiya atakuja kuokoa watu wake. Hakuna mtu atakayewalazimisha tena kutumika kama watumwa au kupigana nao. Habari hizi zilifariji watu wale walioamini (mash. 1-5). Roho Mtakatifu aliwaambia ya kwamba Kristo atazaliwa, na atatawala dunia nzima (mash. 6,7).

Mungu alikuwa ameazibu Israeli, lakini walikataa kujifunza maneno aliyataka kuwafundisha. Adui wao walikuwa wameharibu miji yao lakini Waisraeli walifanya shauri kuijenga tena, na kupanda miti hata mizuri kupita mbele (mash. 8-10). Lakini Mungu alisema atawaazibu hata kupita. Atatumua adui wao kupigana nao (mash. 11,12), na watu wengi watauawa (mash. 13-17). Makabila ya Israeli watapigana na Wamisri na viongozi wao hawataweza kutawala watu wao vizuri (mash. 18-21).

*Shairi gani linatujulisha ya kwamba Mwana wa Mungu atazaliwa kama mtoto mchanga duniani?*

### SURA 10

Isaya alitangaza **ole** au huzuni, juu ya watawala wa Israeli wasiotendea watu masikini kwa haki (mash. 1-4). Mungu atatumika na watu wa Asuria kuazibu Yuda (mash. 5-11), lakini ataazibu Asuria vilevile (mash. 12-19). Vilevile watu wachache wa Israeli wataokolewa (mash. 20-23). Mfalme wa Asuria atakuja toka kaskazini kupigana na watu wa Yerusalema, lakinii Mungu ataharibu majeshi yake (mash. 23-34).

Mara nyingine Mungu anatumika na wasioamini kuazibu watoto wake mwenyewe. Sharti tukumbuke ya kwamba Mungu atatuazibu kila mara tunapofanya zambi. Lakini kama tukirudi karibu na Bwana, hatuhitaji kuogopa adui kwani bila shaka Mungu atatulinda.

*Shairi gani linaonyesha ya kwamba Waasuria walikuwa wenye kiburi?*

## **ISAYA**

### **SURA 11**

Israeli ni kama mti ambao Mungu alikata karibu na udonango. Hata hivi Masiya atatoka kwa kisiki cha mti huu na kuota kuwa kama tawi kubwa (sh.1). Atapakaliwa na Roho ya Mungu (sh.2); atakuwa na akili na haki (mash. 3,4). Atatawala dunia, na wanaume na nyama wakali watacaa pamoja na salama (mash. 5-9). Watu wa mataifa watafika karibu na Kristo namna watu wanavyozunguka bendera yao (sh.10). Wayuda watarudi kwa inchi yao wenyewe na kukaa pale nyuma ya kushinda kwa miaka mingi katika inchi nyingine kama wafungwa (mash. 11-16).

*Wakati gani nyama wakali wataacha ukali wao?*

### **SURA 12**

Halafu watu wa Israeli watashukuru Bwana na kuimba wimbo huu mdogo wa sifa kwa Bwana. Watafurahi sana kwa sababu Bwana hawakasirikii tena (sh.1). Kila mmoja wao anaweza kusema ya kwamba Mungu ni Mwokozi wake (sh.2). Watu watakunywa Maji ya Uzima Bwana tu anayoweza kutoa (sh.3; Yoane 4:13,14). Halafu wataimba sifa kwa Mungu anayejulikana katika dunia yote lakini anayekaa katika Yerusalem (mash. 4-6).

### **SURA 13**

Tumeona ndani ya sura 1-12 ya kwamba itakuwa sharti kwa Mungu kuhukumu Israeli kwa zambi zao. Sasa tutasoma juu ya hukumu yake kwa mataifa mengine:

Babeli, sura 13, 14, 21

Moabu, sura 15, 16

Damasiki, sura 17

Inchi moja ngambo ya Etiopia, sura 18

Misri, sura 19, 20

Duma na Arabia, sura 21

Yerusalem vilevile, sura 22

## SURA 11-14

Tiro, sura 23

Dunia kwa wakati wa kuja, sura 24

Mungu atatumika na malaika watakatifu kuhukumu Wababeli (au Wakaldea) (13:1-5). Askari za Babeli wataogopa (mash. 6-8), wakati Bwana atakapofanyiza nyota kuwa giza (mash. 9-13). Wababeli wataharibiwa na *Wamedi* (mash. 14-18), na watu hawatapanga katika mji wa Babeli tena **kamwe** (mash. 19-22).

*Mungu ataagiza nani kuharibu Babeli?*

## SURA 14

Waisraeli watarudi karibu na Mungu, na watarudia inchi yao wenyewe tena. Halafu watafanyiza Wababeli kuwa wafungwa wao (mash. 1-3).

Wayuda watazarau mfalme wa Babeli wakati anapoanguka katika Hadeze pahali wafu wanapokaa (mash. 4-8); na watu katika Hadeze watamcheka vilevile (mash. 9-19). Watafanya hivi kwa sababu alikuwa na kiburi nyingi wakati alipokuwa hai; alitaka kuwa sawasawa na Mungu (mash. 13-14).

Watu wa Mfalme wa Babeli watauawa vilevile (mash. 20-23), lakini lilikuwa kusudi la Mungu kuharibu Waasuria kwanza na kufungua watu wake (mash. 24-27). (Isaya alikuwa na ono hili katika mwaka Mfalme Ahaba alipokuwa na Hezekia, mwana wake, alipoanza kutawala, sh.28; 2 Wafalme 16:20). Haifai Wafilstini kufurahi wakati ufalme wa Asuria unapoangamizwa, kwa sababu wao wataangamizwa vilevile. Siku ile Wayuda hawataomba mataifa mengine kuwasaidia tena, lakini watategemea Bwana (sh.32).

Mfalme wa Babeli ni mfano wa Shetani, anayeitwa *Lusifero*, au *Mwana wa Asubui* (mash. 12-15). Shetani alitaka kuwa sawasawa na Mungu ili aweze kutawala juu ya malaika zote, lakini Mungu alimfukuza toka mbingu, na atamtupa katika ziwa la moto; soma Ezekieli 28:11-15; Ufunuo 20:10.

*Nani alitaka kuwa sawasawa na Mungu?*

## ISAYA

### SURA 15

Mungu ataharibu watu wa Moabu vilevile. Moabu ilikuwa inchi ndogo kwa upande wa kusini na mashariki wa Israeli. Watu wa inchi ile walikuwa wazao wa Loti (Mwanzo 19:37) na walikuwa adui wa Waisraeli. Katika usiku mmoja Kiro, mji wa Moabu uliangamizwa (sh.1), kisha kulikuwa na kulia na kulalamika kwa sababu ya huzuni (mash. 2-5). Kwa nini? Kwa sababu hakutakuwa na mvua kwa mashamba (sh.6); watu watakimbia (mash. 7,8), lakini simba wakali watawakamata (sh.9).

### SURA 16

Watu wa Moabu watatuma zawadi kwa Yuda na kuomba Wayuda kuwapa pahali watakapoweza kukaa na salama wakati itakapowapasa kuondoka katika inchi yao wenyewe (mash. 1-5). Mungu ataazibu Wamoabu kwa sababu ya kiburi yao (mash. 6-8); kisha wataombolea na kutoa machozi na Isaya aliwahurumia (mash. 9-11). Sanamu zao hazitaweza kuwasaidia (sh.12), na Mungu atashusha taifa la Moabu chini kabisa. Taabu hii itawapata mbele ya miaka mitatu mingine na watu wachache tu watabaki hai kwa mwisho wake (mash. 13,14).

*Mungu aliazibu Moabu kwa sababu gani?*

### SURA 17

Damasiki ulikuwa mji mkubwa wa Suria, ndiyo inchi ya tatu itakayohukumiwa na Mungu (mash. 1-3). Halafu nabii alisema na Israeli tena, akawaambia ya kwamba Mungu atahukumu Israeli vilevile (mash. 4,5). Wengine wa watu watarudi karibu na Bwana nyuma ya kupata mateso ya kutosha (mash. 6-8), lakini wengine wataazibiwa kwa sababu walikuwa wamesahau Mungu (mash. 9-11). Waasuria wengi walikuja kupigana na watu wa Yerusalem, lakini Mungu aliwaharibu katika usiku mmoja tu (mash. 12-14; 37:36).

Manabii walisema tena na tena juu ya siku kubwa moja iliyo kwanza mbele, inayoitwa Siku ya Bwana.

## **SURA 15- 20**

Siku ile wenye zambi watahukumiwa na wale wanaopenda Bwana watapata furaha kubwa. Ndani ya sura hii tunasoma juu ya hukunu ya Mungu (mash. 4,9) , lakini wengine wataamini Bwana (sh.7).

*Mashairi gani ndani ya sura hii yanatupasha juu ya hukumu ya Mungu kwa Damasiki?*

## **SURA 18**

Nabii alipasha juu ya hukumu ya Mungu kwa inchi moja kwa upande wa kusini wa Etiopia. Inchi hii ilituma wajumbe kwa Israeli wakati Israeli ilipoharibiwa na adui. Mungu ataita mataifa mengine kusaidia ndani ya kazi ya kurudisha Waisraeli kwa inchi yao. Watatoa watu wa Mungu kama sada-ka kwake (sh. 7).

## **SURA 19**

Inchi ya Misri itapata taabu nyingi vilevile. Wamisri watapigana katikati yao (sh.2), na miungu yao haitaweza kuwasaidia (mash. 1,3). Mungu ataruhusu mfalme wa inchi nyingine kutawala Misri (sh.4). Mto Nili utakauka (sh.5), na watu hawataweza kupata samaki tena (mash. 6-8), wala kufanya kazi namna nyingine (mash. 9,10,15). Viongozi vyta Misri hawatajua nini inawapasa kufanya kwa kusaidia inchi yao (mash. 11-14,16,17). Lakini Mungu aliahidi kubariki Wamisri na Waasuria wakati watakapogeuka kwake; neno hili litatokea wakati Kristo atakapokuja tena kutawala dunia (mash. 18-25).

## **SURA 20**

Hata leo kuja kwa Kristo mara ya pili ni kwanza mbele, lakini kwa wakati ule Mungu alisema na Isaya kuondosha viatu vyake na mengine ya mavazi yake, ili aweze kuonekana kama mtu aliyefungwa wakati wa vita. Hii ilikuwa alama kwa Misri na kwa Etiopia, kwa sababu mfalme wa Asuria atawa-ondosha kama alivyofanya na watu wa Asidodi (mash. 1-4).

## **ISAYA**

Halafu watu wa Yuda watajifunza ya kwamba ni upumbavu kabisa kutegemea Misri au Etiopia (mash. 5,6).

*Kwa nini Isaya aliondoa viatu vyake na mengine ya mavazi yake?*

### **SURA 21**

*Mzigo* ni unabii juu ya hukumu na tunaona mizigo mitatu namna hii katika sura 21.

1. Jangwa la bahari ndiyo inchi ya Babeli (sh.1). Elamu (au Persia) na Wamedi watashinda Babeli (sh.2). Isaya aliogopa sana wakati Bwana alipomwonyeshea nini itatokea (mash. 3,4). Watawala wa Babeli walikuwa wakikula karamu, lakini zamu aliona majeshi ya Wamedi wakikaribia mji (mash. 5-10).

2. *Duma*, ni jina lingine kwa Idumea au Edomu. Watu wa Edomu waliogopa Waasuria na mmoja wao aliuliza Isaya kama hatari ilikuwa karibu kupita. Nabii alimwambia ya kwamba asubui itafika nyuma kidogo na Waisraeli watacaa na salama, lakini kwa watu wa Edomu usiku ulikuwa ukikaribia nao wataharibiwa. Wengine wa wanaume wa Edomu walitaka kujuua kweli kweli, hivi Isaya alisema nao kumwuliza tena nyuma (mash. 11,12).

3. Nabii aliwaambia Waarabia ya kwamba Mungu atawa-azibu, lakini hatawaharibu pia (mash. 13-17).

### **SURA 22**

*Bonde la ono* ndilo Yerusalem. Ingalipasa watu wa pale kuhuzunika kwa sababu Mungu atatumua Waasuria kupigana nao. Lakini hawakuhuzunika. Walikuwa wakijifurahisha na maneno ya dunia (mash. 1-3). Isaya aliwaambia tena ya kwamba walikuwa karibu kupata matata (mash. 4-7), lakini watu wa Yerusalem walifanya mashauri wao wenyewe kuzuiza adui wasiingie mjini mwao (mash. 8-14).

## Sura 20 - 24

Sebuna, mchunga mali, alikuwa na kazi kubwa mjini na Bwana alitangaza ya kwamba atatupwa katika inchi ya Babeli, na kufa pale (mash. 15-19). Eliakimu alikuwa mfano wa Bwana Yesu na Mungu alimheshimu mjini (mash. 20-25).

Bwana Yesu ni kama msumari wa nguvu kwa sababu tunaweza kumwamini na kumtegemea. Alikatwa chini wakati alipokufa kwa zambi zetu, lakini sasa Mungu amempa utukufu mkubwa.

*Nani alikomboa Sebuna kwa kazi yake kama mchunga mali katika Yerusalem?*

### SURA 23

Watu wa biashara walisafiri ndani ya merikebu zao toka Tarsisi, ndio mji wa Espagne, inchi ya mbali sana. Kila mara walifanya biashara nyingi katika Tiro, mji mkubwa kwa Bahari ya kati. Mara hii walifikia Kitimu, ndicho Kipuro, kisanga kilichokuwa karibu na Tiro, wakati waliposikia ya kwamba watu wa Tiro walikuwa wameshindwa vitani. Kwanza Wababeli waliharibu Tiro, lakini nyuma ya miaka 70 mji ulijengwa tena na watu wa mji walianza kufanya biashara tena (mash. 15-18). Mwishoni Wayuda waliharibu. Labda shairi 18 limetimizwa kwa sehemu, lakini litatimizwa kabisa kabisa kwa wakati wa kuja.

### SURA 24

Sura hii inapasha juu ya siku ya kuogofya ya Bwana wakati Mungu yeye mwenyewe atakapohukumu inchi ya Israeli (mash. 1-4) kwa sababu ya zambi za watu wa inchi (mash. 5-6). Watu wengi watakuwa, na wale watakaopona watakuwa na huzuni nyingi (mash. 7-12). Wengine katikati yao watatukuza Bwana (mash. 13-16). Wengine wataponea hatari moja, lakini watapatwa na hatari nyingine (mash. 17-20). Bwana atahukumu roho wachafu vilevile, na wafalme wa dunia (mash. 21,22) na mwishoni atatawala kama Mfalme katika Yerusalem (sh.23).

*Nani atatawala kama mfalme katika Yerusalem?*

## ISAYA

### SURA 25

Sura 25, 26, na 27 zimeitwa Kitabu cha Nyimbo, kwa sababu Waisraeli wataimba sifa kwa Mungu. Hapa tunaona ya kwamba taifa la Israeli watasifu Bwana kwa sababu aliwaokoa na kuwarudisha karibu naye (mash. 1-8). Masiya atafanya karamu kubwa (sh.6), na kila alama ya huzuni yao itapotea (sh.7). Shairi 8 linapasha juu ya Kristo aliyeshinda mauti kwa njia ya ufufuko wake. Mungu atashusha adui wa Israeli chini kabisa (mash. 9-12).

Mungu atafanya karamu kubwa kwa watu wote,  
naye ametuagiza kuwaita kufika kwa karamu hii  
(Matayo 22:2,3,9).

### SURA 26

Watu wa Yuda wataimba wimbo huu wakati watakapo-rudi kwa inchi yao (mash. 1,2). Wao wote wataweza kusema ya kwamba Mungu aliwaokoa toka adui wao (mash. 3-9). Lakini watu wasiookolewa watakuwa waovu hata wakati Kristo atakapotawala dunia hii (mash. 10,11). Watu wa Mungu walikiri ya kwamba walilazimishwa kutii watu, lakini Mungu alikuwa ameharibu adui wao (mash. 13-15). Watu wa Yuda walikuwa na huzuni kwa sababu hawakuzalia Mungu matunda (mash. 16-18). Lakini Mungu aliwafariji, kwa njia ya kuwaambia ya kwamba taifa lao litaishi tena (sh. 19). Mungu alisema na watu wake kujificha wakati alipoharibu adui wao (mash. 20,21).

*Kutakuwa na watu waovu duniani wakati Bwana Yesu  
atakapotawala kama Mfalme?*

### SURA 27

Shairi la kwanza linatupasha habari za nyama wakali watatu wanaoishi ndani ya maji; wao ni mifano ya watawala wa adui wa Israeli watakaoazibiwa na Mungu.

Mungu atalinda watu wake, ndio Waisraeli (mash. 2-5), na

## SURA 25 – 28

kuwafanyiza kuwa baraka duniani (sh.6); lakini alisema hatasimamisha taifa lenyewe tena kufika wakati watu walipokwisha kuharibu sanamu zao (mash. 7-9). Wayuda wengine hawataamini Mungu kamwe (mash. 10,11), naye atawaazibu. Lakini wengine wa Waisraeli wataishi ndani ya inchi nyingi, toka mto mkubwa, ndio Furati, kufika mto mdogo wa Misri, na Mungu atawakutanisha tena (mash. 12,13).

## SURA 28

Tunaweza kuita sura 28-35 *Vitabu vya Ole* (28:1; 29:1,15; 30:1; 31:1; 33:1). Sura hizi zilijulisha Wayuda waziwazi ya kwamba haifai waasi Waasuria na kutegemea Wamisri kuwasaidia. Bwana alionya watu wa Yerusalem ya kwamba wata-pata matata mengi kwa sababu walikataa kuamini maneno ambayo Isaya aliwaambia, lakini nyuma atawaokoa. Sura hizi zinatazama mbele vilevile kwa siku za mwisho wakati Mungu atakapoharibu kila mtu anayekataa kumtii.

Ole ya kwanza ilikuwa kwa Efuraimu wanaoitwa *taji ya kiburi* (sh.1). Waasuria watakuja mbio na kukamata inchi nzima (mash. 2-4), lakini Waisraeli wengine watageuka kwa Bwana naye atawabariki (mash.5-6).

Isaya alionya watu wa inchi yake tena na tena wasinywe mvinyo nyingi zaidi (5:11,22; 28:1,3,7; 56:12). Sharti tukumbuke ya kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya miili yetu na kwa sababu hii haifai kwetu kula vyakula vingi zaidi wala kuvuta tumbako, kunywa malofu au kumeza dawa itaka-yoharibu miili yetu (Waroma 12:1).

Kisha Isaya alisema na watu wa Yuda (mash. 7-29). Walikuwa wamefanya zambi kubwa (mash. 7,8) na walicheka Isaya kwa sababu habari ambazo aliwaletea toka Mungu zilikuwa nyepesi kufahamu (mash. 9,10). Hivi Mungu alisema atasema nao kwa lugha ya inchi nyingine, ndiyo lugha ya Waasuria

## ISAYA

(sh.11). Watu wa Yuda walitegemea agano ambalo walifanya na taifa lingine (mash. 14,15). Lakini haifai wategemee watu wengine kwa sababu watu wale watawapungukia tu. Iliwapasa kutegemea na kuamini Kristo tu kwani yeze hatawapungukia kamwe (mash. 16-22). Watu wanajaribu kufanya mashauri bila kuomba Mungu kuwaongoza, lakini mwisho wa kufanya hivi ni kama kitanda kilicho kifupi zaidi kwa mtu mwenye kuchoka kuweza kupumzika vizuri. Akili ya watu haiwezi kusaidia kwa wakati wa hatari.

Halafu Isaya alikumbusha wasikiaji wake ya kwamba mlimaji shamba anafanya maneno mbalimbali kwa wakati mbalimbali. Vivyo hivyo Mungu hafanyi kazi yake sawasawa kila mara lakini anatumika kwa njia mbalimbali. Haazibu watu wake saa zote (mash. 23-29).

Mungu anatuazibu, lakini kusudi la azabu hii ni kutusafisha kwa roho. Mungu aliazibu Daudi wakati alipofanya zambi na halafu Daudi alikaa na ange juu ya maneno ya wanawake hata mwisho wa maisha yake (2 Samweli 12:14).

*Nani ndiye Jiwe la damani ambaye tunaweza kumtegemea kabisa (sh.16)?*

## SURA 29

Arieli ni jina lingine kwa Yerusalem, na majeshi ya Waasuria watauzunguka (mash. 1-4). Watakuwa karibu na kushinda na kukamata mji, lakini kwa mwisho Mungu atawa haribu (mash. 5-8). Waasuria watakuwa kama mtu anayeota ndoto: anafikili ana vyakula vya kutosha, lakini anaamka toka usingizi mwenye njaa. Waasuria watafikili walikuwa wameshinda, lakini wataharibiwa gafula.

Watu wa Yuda hawatapokea habari hizi za nabii wa Mungu, na hawatati Mungu (mash. 9-14); hivi tunasoma juu ya ole nydingine kwa watawala wa Yerusalem. Walikuwa wakifanya mapatano na Misri, wakizania Mungu hatajua neno

## **Sura 28 – 31**

hili (mash. 15-17). Lakini kwa siku ya Bwana kutakuwa na baraka kubwa (mash. 18-24).

### **SURA 30**

Halafu kuna ole kwa watu wa Yuda waliojaribu kufanya mapatano na Misri kupigana na Asuria (mash. 1,2). Lakini Wamisri watashindwa, na Wayuda watapata haya (mash. 3-5). Nyama wakali watatesa wajumbe kwa safari yao kwenda Misri, na safari yao haitakuwa na faida (mash. 6,7). Bwana alisema walikuwa wakimwasi yeye (mash. 8,9), na kukataa kusikiliza manabii wake (mash. 10,11). Kwa sababu hii Mungu atawaharibu gafula (mash. 12-14).

Watu wa Yuda watapata raha kama wakigeuka kwa Bwana, lakini kama wakikaa kutegemea majeshi yao, hawatashinda (mash. 15-17).

Bwana alisema atangoja kufika wakati watakapokwisha kujifunza neno hili, kisha atawatendea kwa neema (mash. 18-20). Atawaonyeshea njia yake nao watatupa sanamu zao (mash. 21,22). Mungu atabariki inchi yao sana wakati Kristo atakaporudi (mash. 23-26). Watu wa Israeli wataimba kwa furaha (mash. 27-29) wakati Bwana atakapoharibu jeshi la Asuria (mash. 30-33).

*Shairi gani ni ahadi ya kwamba Mungu atatuonyeshea njia ya haki?*

### **SURA 31**

Waisraeli walitaka kuomba Wamisri kuwasaidia, lakini kwa njia hii walionyesha ya kwamba hawakuamini Mungu aliweza kuwaokoa. Wamisri walikuwa watu tu na Mungu atawahukumu vilevile (mash. 1-3). Bwana aliahidi kuponyesha Yerusalem toka mikono ya Waasuria (mash. 4,5, 8,9). Aliita watu kugeuka kwake, na kutupa sanamu zao zote (mash. 6,7).

Mungu haahidi ya kwamba hatutapata matata

## ISAYA

kamwe, lakini anaahidi kuwa pamoja nasi wakati wote (Waebrania 13:5). Ingetupasa kutegemea Bwana kwa pahali pa kuomba watu wa dunia kutusaidia. Misri (31:1) ni mfano wa dunia.

### SURA 32

Roho Mtakatifu anatupasha hapa juu ya watu watakaoishi ndani ya ufalme wa Kristo. Kristo Mfalme, atatawala kwa haki, na kulinda watu wote wanaofika kwake (mash. 1,2). Maisha ya watu yatakuwa marefu kupita nao wataweza kufahamu maneno vizuri kupita (mash. 3,4). Watu wema wataitwa wema na watu wabaya (mash. 5-8).

Bwana alionya wanawake wa Yerusalem na kuwaambia ya kwamba watapata matata mengi (mash. 9-14). Kisha aliwatiroho nguvu kwa njia ya kuwapasha maneno mengine juu ya ufalme wake kwa wakati wa kuja. Roho Mtakatifu atamimiwa juu ya watu, na serikali yao watatenda kwa haki (mash. 15,16). Ni kusema watu wote wataweza kukaa na kutumika na salama (mash. 17-20).

*Nani atalinda watu wote wanaokuja kwake?*

### SURA 33

Askari wa Waasuria walikuwa wakali sana na shairi 1 linataja ole juu yao. Nyuma kidogo watateswa wao wenyewe namna walivyotesa Waisraeli.

Kisha watu waliimba wimbo wa maombi na sifa kwa Bwana. Ona maombi yao ndani ya shairi 2 na jibu la Mungu ndani ya mashairi 3 na 4; na sifa yao ndani ya mashairi 5 na 6. Walikuwa wamepata taabu kubwa (mash. 7-9) lakini Bwana alikuwa amewasaidia (mash. 10-12). Atashinda adui wake mbio na kuwapa watu wenye haki zawabu (mash. 13-16). Wataona Mfalme, Bwana Yesu Kristo (sh. 17) na hawatawaza tena juu ya taabu yao ya mbele (mash. 18,19). Wataona Yerusalem vilevile, ndio mji wa Bwana (mash. 20-24).

## SURA 31 – 36

### SURA 34

Hapa Mungu aliita mataifa kusikiliza, na aliwaambia juu ya hukumu ambayo itawapata (mash. 1-4). Kisha alitangaza ya kwamba atahukumu watu wa Edomu, inayoitwa Duma katika 21:11. Kutakuwa na vita (mash. 5-7), na moto (mash. 8-10); nyama wakali tu wataishi inchini mwa Edomu (mash. 11-15). Mungu atatimiza maneno yote watumishi wake wanayotabiri (mash. 16-17). Kwa wakati wa sasa hali ya inchi ya Edomu ni kweli namna Isaya alivyotabiri ndani ya mashairi haya.

*Edomu itaharibiwa kwa moto usiokwisha kamwe. Neno  
hili ni mfano wa nini?*

### SURA 35

Sura hii fupi inapasha juu ya ufalme wa utukufu wa Masiya. Kutakuwa na vyakula vyta kutosha kwa sababu jangwa litakuwa kama shamba (mash. 1,2). Watu watakuwa wenye nguvu na wahodari (mash. 3,4). Wale waliokuwa vipo-fu wataona na macho yao, na viwete wataweza kukimbia na kuruka. Watu wasioweza kusema mbele wataweza kuimba (mash. 5,6). Inchi itabarikiwa (mash. 7-9), na watu wa Mungu wataimba sifa kwake (sh.10). Kweli siku Bwana atakapokuja itakuwa siku ya furaha na ajabu!

### SURA 36

Kitabu cha Isaya kiliandikwa kama wimbo, lakini sehemu kubwa ya sura 36-39 iliandikwa kama historia. Sura hizi zinapasha juu ya maneno yaliyopata Mfalme Hezekia na zinafanana sana na 2 Wafalme 18:13,17 kufika 20:19. Lakini Mfalme Hezekia aliandika mashairi 9-20 ya sura 38 kama wimbo na hatuoni maneno haya ndani ya 2 Wafalme.

Ndani ya sura 36, mfalme wa Asuria alituma Rabashake, mmoja wa maakida wake, kusema na watu wa Yuda wajitoe kwa mfalme wa Asuria (mash. 1-5). Alisema haifai wategemee Misri au Bwana (mash. 6,7).

Aliahidi kuwapa farasi 2000 kama wakiwa na askari za

## ISAYA

kutosha kutemba juu yao (mash. 8,9). Neno hili linaonyesha ya kwamba jeshi la Hezekia lilikuwa dogo sana. Rabashake alisema ya kwamba Mungu ndiye ambaye alimtuma kuharibu Yerusalem (sh.10).

Watumishi wa Hezekia waliomba Rabashake kusema kwa lugha nyingine ili watu wa mji wasiweze kufahamu (sh.11), lakini Rabashake alikataa kwa sababu alitaka watu wa mji wamsikie ili waweze kukataa kutii Hezekia tena (mash. 12-16). Alitaka watoke mjini na kufika karibu naye na aliahidi kuwapeleka kwa inchi nyingine ilioyo kama inchi yao wenyewe (sh.17). Alisema Bwana si mzuri kupita miungu ya mataifa mengine na hataweza kuwaokoa (mash. 19,20). Watu wa Hezekia hawakujibu Rabashake, lakini walikwenda kumwambia mfalme habari hizi zote (mash. 21,22).

Akida wa Saniharibu alijaribu kuharibu imani ya watu wa Yerusalem wasiamini Mumgu tena. Mtu huyu ni mfano wa Shetani anayeingiza mafikili mabaya ndani ya nia zetu kusudi tuwe na shaka juu ya mapendo ya Mungu kwa sisi.

*Kwa nini akida Mwasuria alisema kwa kiebrania?*

## SURA 37

Mfalme Hezekia alisumbuka sana rohoni wakati aliposikia habari hizi na alituma maakida wake karibu na nabii Isaya (mash. 1,2). Mfalme alisihi Isaya kuombea watu waliobaki mjini (mash. 3-5). Isaya alisema naye ya kwamba haifai aogope kwa sababu Rabashake, akida wa Saniharibu, atarudi kwa inchi yake nyuma kidogo (mash. 6,7). Rabashake alituma barua tena karibu na Hezekia kusema Bwana si mkubwa kupita miungu ya mataifa (mash. 8-13). Hezekia aliingia hekalu, akatandika barua yenye mbele ya Bwana, akaomba Bwana kumponyesha kwa utukufu wake mwenyewe (mash. 14-20). Isaya alimwambia Hezekia ya kwamba Mungu atawalinda kwa sababu alijua ya kwamba watumishi wa Saniharibu wali-kuwa wametukana jina lake (mash. 22-25). Waasuria

## SURA 36 – 38

walikuwa wameshinda mataifa mengi kweli, lakini alikuwa Mungu ambaye aliwawezesha kufanya hivi (mash. 26,27). Sasa Mungu atawalazimisha kurudi kwa njia waliyokuja (mash. 28,29). Mungu aliahidi Waisraeli vilevile ya kwamba watakuwa na vyakula nya kutosha nyuma ya kuondoka kwa Waasuria (mash. 30-35). Mungu alituma malaika wake kuharibu Waasuria 185.000 usiku mmoja, na nyuma yake jeshi la Asuria liliondoka (sh.36). Saniharibu aliuawa yeze mwe-nyewe — wana wake walimwua (mash. 37,38).

*Kwa nini Mungu aliua Waasuria 185.000 kwa usiku mmoja?*

## SURA 38

Ndani ya sura 36 na 37 tuliona Hezekia akishinda kwa maneno ya roho na akionyesha ya kwamba alikuwa na imani ya nguvu. Lakini ndani ya sura 38 na 39 Mungu alimpima tena na mara ile hakushinda vizuri.

Kwanza Hezekia alipata ugonjwa wa nguvu, na Isaya alimjulisha ya kwamba atakufa. Ingalipasa Hezekia kunyenyeka mapenzi ya Mungu ndani ya neno hili, lakini Hezekia alisihi Mungu kumponyesha (mash. 1-3). Mungu aliongeza urefu wa maisha yake na miaka 15, na kama alama ya neno hili alirudisha nyuma kivuli cha madaraja kilichosuka kwa madaraja ya Ahazi kwa jua, madaraja kumi, maana yake kurudisha saa nyuma kwa dakika 40. Walitumika na madaraja ya Ahazi kwa kujua kama ni saa ngapi, hivi kwa alama hii Mungu alirudisha nyuma sehemu ya maisha Hezekia aliokwisha kuishi (mash. 4-8).

Hezekia alisifu Bwana kwa neno hili (mash. 9-20). Alifikili atakufa (mash. 10-14), lakini alishukuru Bwana (mash. 15-17), na aliahidi kumsifu milele (mash. 18-20). Basi Isaya alimwambia nini ilimpasa kufanya aweze kupona (sh.21; 2 Wafalme 20:7).

Miaka mitatu nyuma ya maneno haya, Hezekia alizaa mwana mwingine, ndiye Manase, na mwana

## ISAYA

huyu aligeuka mfalme wakati Hezekia alipokufa. Manase alitawala Yuda kwa miaka 55, muda mrefu kupita mfalme ye yote mwengine, lakini alikuwa mwovu sana, kupita wafalme wa mataifa mengine. Manase alitubu yeye mwenyewe, lakini alikuwa amekosea watu wa Yuda sana (2 Mambo 33:1-13). Labda haikuwa vizuri kwa Hezekia kuomba namna alivyoomba. Ingetupasa kuomba tu kwa mapenzi ya Mungu kufanywa katika maisha yetu, si mapenzi yetu wenyewe.

*Hezekia alifanya nini aweze kupona toka ugonjwa wake?*

## SURA 39

Ndani ya sura hii tunaona Mungu akipima Hezekia tena. Mwana wa mfalme wa Babeli alituma wajumbe na zawadi karibu na Hezekia, kwa sababu alikuwa mgonjwa na alipona (sh.1). Kwa wakati ule Babeli lilikuwa taifa la kujulikana hata kama lilikuwa dogo kupita taifa la Asuria, lakini nyuma ya miaka michache Wababeli walishinda Waasuria. Hezekia ali-jivuma kwa sababu mwana wa mfalme wa Babeli alimfikili, akaonyeshea wajumbe hazina zake zote (mash. 1,2). Isaya, mtu wa Mungu, aliuliza mfalme juu ya neno hili, kisha alimwambia ya kwamba Wababeli hawa watamwondolea mali yake yote (mash. 3-7). Neno hili lilitokea kweli kwa wakati wa Yeremia. Hezekia alinyenyeka azabu ya Bwana na ameleta asante kwa sababu taifa lake litakuwa na salama kwa wakati yeye alipokuwa kwanza hai (sh.8).

*Kwa nini Hezekia alionyeshea wajumbe wa inchi nyingine hazina zake zote?*

## SURA 40

Sasa tunaanza sehemu nyingine ya kitabu cha Isaya. Sehemu ya kwanza, sura 1 kufika 35, ilikuwa zaidi juu ya zambi na hukumu; sehemu ya mwisho, sura 40 kufika 66, ni zaidi juu ya Masiya, na baraka Mungu atakazotoa wakati

## SURA 38 – 41

Masiya atakapokuja kutawala. Sura 40 kufika 48 zinafundisha ya kwamba haifai kwa watu wa Mungu kuabudu sanamu.

Ndani ya sura 40 tunaona Mungu akifariji watu na akiahidi ya kwamba Masiya atakuja (mash. 1-11). Roho Mtakatifu alipasha juu ya Yoane Mbatizaji (mash. 3-5; Luka 3:4-6). Sharti Waisraeli wajitayarische kwa kuja kwa Kristo, kwa njia ya kukumbuka ya kwamba wao ni watu tu, lakini Neno la Mungu litasimama kwa milele (mash. 6-8). Bwana ye ye mwenyewe atakuja kutawala, kutoa zawabu, na kulinda watu wake namna mchungaji anavyolinda kondoo zake (mash. 9-11).

Yoane Mbatizaji alikuwa mtu mkubwa sana, lakini alijua ya kwamba Bwana Yesu Kristo alimpita mbali kwa ukubwa, na alisema na watu kufuata Bwana Yesu. Alisema maneno ya kweli tu juu ya Bwana (Yoane 5:33; 10:41).

Huyu ndiye Mungu mkubwa aliye juu ya dunia na mataifa yote (mash. 12-17). Yeye ni mkubwa kupita miungu mingine, na wafalme wote wa dunia (mash. 18-25). Atawapa uwezo waamini wote ambao wanamngojea (mash. 26-31).

## SURA 41

Ndani ya sura hii Mungu aliuliza watu kama uwezo wake ulikuwa mkubwa kupita au mdogo kupita uwezo wa sanamu. Alisimamisha mtu aliyetoka kwa inchi nyingine iliyokuwa kwa upande wa mashariki wa Yuda (mash. 2-4). Sanamu hazikuweza kuponyesha mtu ye yote (mash. 5-7). Mungu alipenda watu wake, ndio Waisraeli, na aliwasaidia kupita sanamu. Alionyesha neno hili kwa Yakobo na Abrahamu na wazao wao (mash. 8,9). Aliahidi kuwasaidia (sh.10), na kuwawezesha kushinda adui wao (mash. 11-16). Atawapa maji kwa kunywa (mash. 17,18), na kugeuza jangwa kuwa mwitu wa miti (mash. 19,20). Sanamu za Israeli hazikuwa-chunga kamwe na mapendo namna hii.

## ISAYA

Sanamu zinaweza kujulisha watu nini itatokea kwa wakati wa kuja? Sivyo, Mungu tu anaweza kufanya hivi. Hapa Mungu aliwaambia ya kwamba Kiro atakuja na kuokoa watu wa Mungu (mash. 21-29; 45:1).

Mara nyine manabii wa uwongo wanaweza kusema mbele nini itatokea kwa wakati wa kuja, lakini haifai tuwaamini kama wakituagiza kuacha kuabudu Mungu, na kufuata mtu fulani (Torati 13:1-3).

## SURA 42

Mtumishi wa Bwana ndani ya mashairi 1-17 ni Masiya. Yeye ni mpole na mwenye neema (mash. 1-4; Matayo 12:18-21). Mungu Mwumba wa wote ameita Masiya kuwa baraka kwa watu (mash. 5-7). Tunaona tena ndani ya mashairi 8 na 9 ya kwamba Bwana ni mkubwa kupita sanamu zote, hivi Roho Mtakatifu anasema na watu wote kuimba wimbo mpya kwa Bwana (mash. 10-12). Bwana mwenyewe atakuja kuharibu adui zake (mash. 13-15), na kuokoa watu wake (mash. 16,17).

Ndani ya mashairi 18-25 mtumishi ndio Israeli, watu wa Mungu. Ingaliwapasa kuwa wajumbe wake, lakini hawaku-timiza kazi hii vizuri.

*Mashairi gani ndani ya Agano Jipyä yanahakikisha ya kwamba mashairi 1-4 yanasema juu ya Kristo?*

## SURA 43

Mungu aliumba watu wake Israeli, na aliahidi kuwa pamoja nao na kuwalinda kwa wakati wa matata, na kuwarudisha kwa inchi yao wenyewe (mash. 1-7). Kisha Bwana aliuliza tena kama sanamu ziliweza kweli kujulisha watu maneno gani yatakayotokea kwa wakati wa kuja (mash. 8,9). Watu wa Bwana wanaweza kutoa ushuhuda ya kwamba yeye ni Mungu wa pekee wa kweli (mash. 10-12); na hakuna mtu anayeweza kuzuiza kazi yake (sh.13). Hapa alitabiri ya kwamba ataleta Israeli tena kwa inchi yao wenyewe nyuma ya kuwa wafungwa katika Babeli (mash. 14-21). Lakini watu

## SURA 41 - 45

walikataa kumwabudu (mash. 22-24). Hata hivi Mungu alikuwa tayari kuwarehemu na rehema yake ni kubwa kupita hukumu zake (mash. 25-28).

*Bwana aliita taifa gani washuhuda wake?*

## SURA 44

Mungu aliahidi tena kubariki watu wake Israeli (mash. 1-5). Alitoa Roho Mtakatifu (sh.3), siku ya Pentekote, lakini atatimiza ahadi hii kabisa kwa wakati wa kuja kwa Bwana. Tunaona tena ya kwamba Bwana ni mkubwa kupita sanamu kwa sababu anaweza kujulisha watu maneno yaliyo karibu kutokea (mash. 6-8).

Halafu Isaya alionyesha ya kwamba watu wanaofanya sanamu ni wapumbavu kabisa (mash. 9-20).

1. Yule anayefanya sanamu ni mtu tu, mwenye kuchoka yeye mwenyewe.
2. Sanamu inafanywa toka mti, na baki la mti wenyewe linatumwiwa kuwashaa moto.
3. Sanamu haiwezi kujiokoa yenye na haiwezi kusaidia mtu.

Halafu Mungu aliagiza taifa la Israeli kumheshimu yeye, kwa sababu alikuwa amewakomboa; aliwaumba na kuvalinda, naye atawapa tena mji wao, ndio Yerusalem (mash. 21-27). Ndani ya shairi 28, Mungu alijulisha Isaya jina la mfalme mkubwa wa Persia, ndiye Kiro. Alifanya hivi miaka 150 mbele ya kuzaliwa kwa Kiro.

*Kwa nini ni upumbavu kuabudu sanamu ya mti?*

## SURA 45

Mungu atasimamisha Kiro kusudi aingie Babeli na kufungua watu wa Yuda (mash. 1-8). Labda waamini wa kweli katika Israeli walishangaa kusikia ya kwamba Mungu atatumika na mtu wa taifa lingine kukomboa watu wake kwa

## ISAYA

sababu alikuwa ameahidi ya kwamba mkubwa wa jamaa ya Daudi ataponyesha watu wake. Lakini Mungu ana ruhusa kutumika na mtu ye yote, na haifai kwa sisi watu kumwuliza juu ya maneno anayofanya (mash. 9-13). Kwa wakati wa kuja mataifa watakubali Israeli kuwaongoza (mash. 14-17). Mungu wa pekee aliyeumba dunia anasema wazi kwa watu (mash. 18,19); lakini sanamu haziwezi kujulisha watu nini itatokea kwa wakati wa kuja (mash. 20,21). Mungu anataka watu wa Mataifa kuokolewa, naye ametuagiza kujulisha watu wote ya kwamba Kristo tu anaweza kutuokoa na kutupatisha nguvu (mash. 22-25; Waroma 14:11; Wafilipi 2:10).

Haifai kwetu kubishana na Mungu, au kumwuliza kwa nini anafanya maneno namna anavyotaka, na wakati anapotaka kuyafanya. Alituumba na anaweza kufanya neno lo lote ambalo linampendeza.

*Mungu alikuwa ameahidi ya kwamba mzao wa Daudi ataokoa Israeli. Basi kwa nini alisema Kiro, mtu wa Mataifa, atawaokoa?*

## SURA 46

Beli na Nebo zilikuwa sanamu, na ilipasa watu kubeba sanamu hizi kwa sababu hazikuweza kutembea (mash. 1,2).

Hakuna mtu aliyehitaji kubeba Mungu; ndiyo ni Mungu anayebeba watu wake (mash. 3,4)!

Neno hili ni kweli leo vilevile. Manabii wa dini za uwongo wanabebesha watu mizigo mizito, na kuwambia ya kwamba sharti watumike na nguvu na kutoa mali waweze kuokolewa. Bwana Yesu Kristo tu anatuokoa kwa sababu ya kazi ambayo yeye mwenyewe alifanya, na anabeba mizigo yetu vilevile (1 Petro 5:7).

Halafu Isaya alionyesha tena namna watu walivyofanya sanamu. Lakini hakuna mtu aliyeefanya Mungu; ni Mungu aliyeumba vitu vyote (mash. 5-7). Mungu tu aliweza kujulisha

## SURA 45 – 48

watu nini itatokea nyuma. Hapa alisema ya kwamba ataita ndege ya mwitu toka mashariki (mash. 8-11); ndege huyu alikuwa Kiro (45:1). Halafu Roho Mtakatifu aliita watu tena kurudi karibu na Mungu (mash. 12,13).

*Isaya alionyesha namna gani ya kwamba Mungu ni namna nyiningine na sanamu (mash. 1-4)?*

## SURA 47

Sasa Mungu alionyesha kwa sababu gani ataazibu Babeli. Atatumua Wababeli kuazibu watu wake (39:6), lakini Wababeli walikuwa watu wakali sana na hawatakuwa na rehema (mash. 1-6). Walikuwa wenyewe kiburi vilevile na walifikili ya kwamba hawatapata matata kamwe (mash. 7-11; Danieli 4:30). Zaidi ya ile, walitegemea wachawi, na watu waliotabiri maneno yatakayotokea kwa njia ya kuangalia nyota (mash. 12-15).

## SURA 48

Mungu alikumbusha watu tena ya kwamba hakuna sanamu inayoweza kuonyesha nini itatokea kwa wakati wa kuja (mash. 1-8). Watu wa Israeli walisema walikuwa wakifuata Bwana (mash. 1,2), lakini Bwana alijua ya kwamba wengi wao walitegemea sanamu zao. Itampasa kuwaazibu, lakini hata-wakatia mbali (mash. 9-11). Atawapeleka kwa inchi nydingi, lakini nyuma ataita mtumishi wake Kiro ambaye atawaruhusu kurudi kwao tena (mash. 12-16). Ingaliwapasa kutii Mkombozi wao (mash. 17-19). Kiro atawaruhusu kuondokea Babeli (mash. 20,21), lakini wale wanaoendelea kuabudu sanamu hawatakuwa na salama kamwe (sh.22).

Ndani ya shairi 16 Masiya, ndiye Kristo, anasema.  
Ni ye ye ambaye Mungu alimtuma. Mungu alituma  
Roho Mtakatifu duniani vilevile, hivi ndani ya shairi  
hili tunaona Mungu, Bwana Yesu (Mwana wa  
Mungu), na Roho Mtakatifu (Yoane 14:24,26).

*Mungu alisema, Mimi Bwana ni wa kwanza na mimi ni wa*

## ISAYA

*mwisho (44:6; 48:12). Ni kusema yeye ni wa milele au mwenye haki au mwenye neema?*

### SURA 49

Ndani ya sura 49-53 tunaona Mungu akiazibu watu wake Israeli kwa sababu walikataa kupokea Masiya.

Ndani ya sura 49, Israeli ni mfano wa Masiya, Mtumishi wa Bwana, aliyeita mataifa kusikiliza (mash. 1-4). Masiya atakuwa Mtumishi wa Mungu wakati atakaporudisha Israeli kwa inchi yao na kuokoa watu wa Mataifa (mash. 5,6). Bwana ameagiza ya kwamba wafalme wote watainama mbele ya Masiya (sh. 7), na aliahidi kujibu maombi ya Kristo kwa wakati wa kutimia kwa njia ya kumfufua toka wafu (sh.8). Watu wengi wataishi katika Yerusalem, na Mataifa watasaidia Waisraeli kurudi toka inchi mbalimbali za dunia (mash. 18-23). Watu wa Israeli waliona uwezo na utukufu wa Babeli wakati walipokuwa wafungwa pale, na walifazaika namna gani wataweza kuokolewa (sh.24). Lakini Bwana atawaokoa ili watu wote wajue ya kwamba ndiye anayeokoa Israeli (mash. 25,26).

### SURA 50

Bwana hakuachana na Wayuda namna mume anavyo-achana na mke wake, lakini amewaweka kando kwa sababu ya zambi zao (sh. 1). Mashairi 2 kufika 9 yanatufikilisha maneno makubwa juu ya Masiya: Mungu alitafuta mtu kufanya mapenzi yake, lakini watu wote walikuwa wenye zambi. Kristo tu alikuja kufanya mapenzi ya Baba wake (Zaburi 40:7-8). Watu walimkataa, lakini alikuwa na uwezo wote wa Mungu (mash. 2-3). Kristo alikuwa mtu mkamilifu aliyekuwa na upatano wa karibu sana na Baba wake na aliyejua namna gani kusaidia watu na masemo yake (sh.4). Alitii Baba wake hata kama watu walimtesa na kumwua (mash. 5-7). Kwa sababu hii Mungu alifufua Masiya toka wafu, kuonyesha ya kwamba alimpendeza ndani ya maneno yote (mash. 8,9). Atawaongoza wale ambao wanamwamini (sh.10), lakini watu wengine wanafikili ya kwamba akili yao wenyewe inatosha;

## SURA 49 – 53

watajifunza ya kwamba akili yao ni upumbavu tu (sh.11).

*Saa gani Isaya alijifunza kusema maneno yaliyohitajiwa kwa wakati fulani?*

## SURA 51

Watu wengine katika Yuda watatazamia Bwana kuwokoa, na Mungu aliwatia roho nguvu kwa njia ya kusema nao kukumbuka Abrahamu na Sara (mash. 1-3). Mungu alikuwa amebariki Abrahamu na Sara, na sasa aliahidi kuokoa watu wake kwa milele (mash. 4-8). (Roho Mtakatifu anasema mara ngapi ndani ya sura hii kwa watu kusikia? Andika hesabu ya kila shairi \_\_\_\_\_)

Halafu watu waliita Masiya *mkono wa Bwana* na wali-mwomba kuwaokoa namna Bwana alivyookoa watu wake toka Rahaba, ndiyo Misri (mash. 9-11). Masiya aliwajibu na kusema ya kwamba alikuwa amewaumba na ya kwamba haifai kwao kusahau Mwumba wao kamwe (mash. 12-16). Walikuwa wamekunywa kikombe wakati alipowakasirikia (mash. 17-20), lakini atawaokoa na atakasirikia adui wa watu wake (mash. 21-23).

## SURA 52

Watu wa Israeli watakuwa wafungwa kwa Babeli kwa miaka mingi, lakini kwa mwisho Mungu atawaokoa (mash. 1-2). Watu wa Babeli watawaruhusu kwenda zao kama Wamisri walivyofanya miaka mingi mbele (mash. 3-6). Bwana ye ye mwenyewe atarudi pamoja na wafungwa hawa, nao wataimba sifa kwa Mungu (mash. 7-10). Waliagizwa kuwa safi wakati watakapoondokea Babeli (mash. 11,12).

Halafu Roho Mtakatifu alisema juu ya Masiya (mash. 13-15). Mungu atampa mtumishi wake utukufu, sh.13); lakini kwanza itampasa kuvumilia mateso makali (sh.14). Atawea kusafisha watu wengi, kwa sababu alitoa damu yake kwa ajili yao (sh.15; 1 Petro 1:2).

*Mtumishi wa Mungu ndani ya shairi 13 ni nani?*

## ISAYA

### SURA 53

Sura hii tamu sana inatufundisha maneno mengine juu ya Masiya. Watu wachache tu watapokea habari njema juu ya Kristo (sh.1). Hataonekana namna nyingine na watu wengine, na watu watamzarau na kumkataa (mash. 2,3). Atakufia wenye zambi (mash. 4-6). Wayuda watafikili ya kwamba Mungu alikuwa akimhukumu, lakini Roho Mtakatifu alisema wazi ya kwamba ni sisi watu tulio wenye zambi, na ya kwamba Kristo atakufa kwa zambi zetu.

Kristo alinyamaza wakati watu walipomshitaki (sh.7), na hakuhukumiwa kwa haki. Watu walimfunga juu ya msalaba afe, lakini alikufa kwa zambi za Israeli (sh.8). Alizikwa kaburini, ndilo kaburi la mtu tajiri mmoja (sh.9). Mungu alikubali maneno haya, lakini alifufua Kristo toka wafu. Masiya ataona matunda ya kazi yake na atapendezwa na kutukuzwa sana (mash. 10-12).

Maneno yote yalitokea namna Roho Mtakatifu alivyosema mbele. Kwa mfano, Bwana Yesu alitendewa kama mwenye jeuri, na watu walifikili atazikwa namna watu wengine wenye jeuri walivyozikwa. Lakini sivyo. Yosefu wa Arimatea, mtu wa mali, alizika Kristo ndani ya kaburi lake mwenyewe (Matayo 27:57-60). Ndiyo, Kristo alikufa kwa zambi zetu. Nyuma yake Mungu alimtukuza sana.

*Bwana Yesu atatulia kwa wakati gani?*

### SURA 54

Kabila la Yuda lilikuwa kama mke asiyekuwa na watoto, lakini anayepata furaha wakati mwishoni anapozaa wana na binti. Mungu alisema na watu wa Yuda kuimba kama mwanamke huyu, kwa sababu alikuwa amewaaazibu, na watu wa Yuda walikuwa wafungwa katika Babeli kwa wakati, lakini atawarudisha kwa inchi yao (mash. 1-4). Mungu, Mwumba, ni kama mume kwa Yuda. Aliwaita (mash. 5-8), na alisema hatawakasirikia tena (mash. 9,10).

## SURA 53 – 57

Halafu alisema na watu wa Yerusalem na kuahidi ya kwamba atafanyiza mji huu kuwa mji mzuri sana tena (mash. 11-12). Salama kubwa itajaza Yerusalem wakati adui wake watakapoharibiwa (mash. 13-17).

## SURA 55

Hapa kuna mwito kwa wenyewe kiu. Mungu aliahidi ya kwamba atawapa maji, mvinyo na maziwa, nao hawatahitaji kulipa mali (mash. 1-5). Ndani ya mashairi haya Mungu alikuwa akiita Israeli kuondoka kwa Babeli na kurudia inchi yao wenyewe.

Mashairi haya yanaonyesha vilevile ya kwamba Mungu anataka sana kwa wenyewe zambi kufika kwake na kushibishwa kwa roho. Bwana Yesu alisema maneno namna hii katika Yoane 4:14 na 7:37.

Ndani ya mashairi 6 na 7 Mungu alisema na Waisraeli kurudi kwake. Mawazo yake yanapita mbali mawazo ya mtu ye yote. Bila shaka atatimiza ahadi zake (mash. 8-9), na kurudisha watu wake kwa Yerusalem (mash. 11-13).

*Isaya alisema mawazo ya Mungu ni mbali na mawazo yetu kwa njia gani?*

## SURA 56

Hapa Roho Mtakatifu aliagiza watu kufanya yaliyo haki, na kushika siku ya sabato (mash. 1,2). Kulikuwa na watu wengine wasiokuwa na ruhusa kuingia hekalu la Solonomo, lakini hata wageni na matowashi watabarikiwa katika ufalme wa Kristo kama wakishika maagizo ya Mungu (mash. 3-8). Nyama wakali ni mifano ya wafalme wa mataifa mengine walioweza kupiga vita na Israeli kwa sababu viongozi wa Israeli walikuwa vipofu, au walilala au kulewa (mash. 9-12).

## SURA 57

Mashairi mawili ya kwanza ya sura hii yanaendelea na

## ISAYA

mafundisho ya 56:9-12; viongozi hawakuweka roho juu ya maneno yaliyokuwa yakipata Israeli. Halafu nabii alihukumu watu wa Yerusalem kwa sababu waliabudu sanamu na kufanya zambi (mash. 3-9), na walikataa kurudi karibu na Mungu (mash. 10-13). Lakini Mungu aliahidi ya kwamba atawasamehe, na kuwapa salama kama wakitubu na kuacha kuabudu sanamu zao. Soma sehemu ya mwisho ya shairi 13 pamoja na mashairi 14 kufika 19. Mungu atataabisha wale walioendelea kufanya zambi (mash. 20,21).

Mungu wa milele ni mkubwa, naye ni juu ya yote;  
hata hivi anakubali kukaa pamoja na mtu ye yote  
ambaye anajinyenyewekeza na kukiri ya kwamba yeye  
ni mwenye zambi (sh.15).

*Mungu mkubwa na wa milele anaahidi kukaa pamoja na  
watu wa namna gani?*

## SURA 58

Halafu Bwana alionyeshea Isaya ya kwamba Waisraeli walikuwa wakifunga chakula siku fulani. Walitenda sawa-sawa walipenda Bwana, lakini hata hivi walikuwa wakikwamana na zambi (mash. 1-5). Mungu anataka watu kumwabudu, lakini sharti watembee kwa haki na kusaidia watu wengine. Kama wakifanya hivi, Mungu atawabariki sana (mash. 6-12). Hapa aliahidi kuwabariki sana kama wakishika siku ya sabato (mash. 13-14).

## SURA 59

Nabii alikumbusha watu ya kwamba Mungu hatasikia maombi yao kwa sababu ya zambi zao (mash. 1-2); zambi kama uuaji, na kusema wongo (sh.3), na zambi nyingi nyingine (mash. 4-8). Watu walikubali ya kwamba walikuwa wamefanya zambi kubwa, na ya kwamba hakuna mtu aliyeeweza kuwaokoa (mash. 9-15). Kwa sababu hii Masiya atakuja kuwasaidia. Yeye ni Mwombezi (sh.16), na Mkombozi (sh.20). Atawezesha Waisraeli kushinda adui wao (sh. 18).

## SURA 57 - 62

### SURA 60

Ndani ya sura hii tunaona mji wa Yerusalem kama mji mkubwa wa dunia wakati Kristo atakapokuja kutawala. Watu wa Mataifa watasaidia Wayuda kurudia Yerusalem toka inchi nyingi (mash. 3-9). Mataifa watatumikia watu wa Israeli (mash.10-12), na Mungu atabariki inchi yao sana (mash. 13-16). Kristo atatawala kama Mfalme, na kutakuwa na salama, haki na nuru ya milele (mash. 17-22).

*Shairi gani linaonyesha ya kwamba Mataifa wataleta  
mali yao kwo Yuda?*

### SURA 61

Roho Mtakatifu anapasha juu ya kuja kwa kwanza kwa Kristo ndani ya shairi 1 na sehemu ya kwanza ya shairi 2, lakin ni kwa wakati wa kuja Mungu atalipiza kisasi wale ambao wanamchukia; ona Luka 4:16-21. Masiya atawapa watu wake utukufu, nao watajenga tena miji ya Israeli (mash. 3,4). Mataifa watafanya kazi ya walimaji, lakin ni watu wataheshimu Israeli kwa sababu Mungu aliwachagua kuwa watu wake (mash. 4-9). Waisraeli watafurahi ndani ya Bwana wakati atakapo-warudisha kwake (mash. 10,11).

Bwana Yesu alisoma shairi 1 na sehemu ya kwanza ya shairi 2, wakati aliposimama katika sunagogi kwa Nazareti (Luka 4:16-19). Alikuja mara ya kwanza kufundisha watu juu ya neema ya Mungu (Yoane 1:17). Atakuja tena na kuhukumu watu wote ambao walimkataa (2 Watesalonika 1:7,8).

*Shairi gani linatupasha juu ya kuja kwa kwanza na kuja  
kwa pili kwa Bwana?*

### SURA 62

Nabii alisema ya kwamba hatapumzika kufika wakati alipoona Yerusalem na utukufu mpya (mash. 1-9). Atakaa kuomba ili Mungu aweze kuponyesha mji ule, na ili Kristo

## ISAYA

aweze kurudi kuwa Mfalme. Mungu aliahidi ya kwamba Mataifa wataona utukufu wa Yerusalem (mash. 2,3), na ya kwamba watu watafurahi (mash. 4,5). Ingepasa waamini kuomba kwa Bwana kurudi (mash. 6,7), kwa sababu Mungu aliahidi ya kwamba ataokoa watu wake (mash. 8,9). Mataifa watasaidia Yuda kurudia inchi yao, na watawaita watu watakatifu (mash. 10,12).

### SURA 63

Hapa kuna mfano wa Bwana Yesu wakati atakaporudi na kulipiza kisasi adui wake. Mavazi yake ni mekundu kwa damu ya adui hawa wa watu wake (mash. 1-6). Halafu Roho Mtakatifu alikumbusha Israeli ya kwamba Mungu alikuwa amewabariki mara nyingi kwa miaka iliyopita (mash. 7-14). Alikuwa ametuma malaika yake kuwaokoa, lakini nyuma kidogo walimwasi tena. Hata hivi alikumbuka ahadi zake na kuwafikisha kwa pahali pa raha. Hapa walililia Mungu tena kuwaokoa kwa sababu walikuwa watu wake (mash. 15-19).

*Masiya anaweza kuokoa (sh.1). Basi kwa nini mavazi yake ni mekundu (sh.2)?*

### SURA 64

Watu wa Israeli waliendelea kuomba Mungu kuwaokoa kwa njia ya kutuma Masiya tena (mash. 1-3). Walikuwa tayari kukiri ya kwamba Mungu ni mwenye haki (mash. 4,5), na ya kwamba wao ni wenye zambi (mash. 6,7). Waliomba Mungu kuwahurumia, kuwasaidia, na kuwarudisha kwa Yerusalem (mash. 8-12).

### SURA 65

Hapa Roho Mtakatifu alionyesha vizuri sana mapendo na wema wa Mungu kwa watu ambao walimwasi na kuabudu sanamu (mash. 1-7). Kutakuwa na baki la taifa la Israeli watakaoamini Bwana, na Mungu atawaponyesha wasife (mash. 8-10). Wale wanaokataa Masiya watakuwa vitani (mash. 11-16).

## SURA 62 – 66

Wakati Kristo atakapokuja tena atatawala dunia kwa miaka elfu moja. Ndani ya sura hii Mungu aliahidi kuumba mbingu na dunia mpya, na watu wote watakuwa na furaha (mash. 17-19). Watu wataishi miaka mingi na kugeuka wazee sana (mash. 20-22), na Mungu atajibu maombi yao mbio (sh.24). Nyama wakali hawataua wala kula nyama wengine (sh.25).

## SURA 66

Mungu alifundisha ya kwamba alichukia sadaka watu walizotoa wakati maisha yao yasipokuwa safi na matakatifu. Alikuwa ameagiza watu wake kuleta sadaka namna alivyo-agiza ndani ya sheria yake, lakini sharti wale wanaofanya hivi watembee kwa usafi (mash. 1-4). Watu hawa waaminifu wata-chukiwa na ndugu zao (sh.5), lakini Bwana ataonekana katika Yerusalem kuazibu adui zake, na kurudisha taifa la Israeli ndani ya siku moja (mash. 7-14).

Roho Mtakatifu anaonyesha ya kwamba Bwana ataharibu adui zake kwa moto (mash. 14-18). Halafu Israeli watapasha habari za utukufu wa Kristo kwa dunia nzima: soma sehemu ya mwisho ya shairi 18, na mashairi 19 kufika 23. Halafu Mataifa watakuja pamoja na Wayuda kuabudu kwa Yerusalem. Adui za Kristo watauawa, na watu watakumbuka kwa milele hukumu iliyowapata (sh.24). Hili ndilo onyo la mwisho la unabii wa Isaya.

Isaya alitabiri juu ya Masiya kupita mwandishi ye yote mwingine katika Agano la Kale.

*Mashairi gani ndani ya sura 65 na 66 yanasema juu ya mbingu na dunia mpya?*

## **Majibu kwa Maulizo**

### *Sura*

1. Anaweza kama akiamini Neno la Mungu (sh. 18).
2. Kwa sababu wataishi kwa muda mfupi tu (sh.22).
3. Mbili, na sita nyingine ndani ya sura 5.
5. Waamuzi wamelewa na watu waliwapa mali wasiwahuku mu (mash. 22,23).
6. Aliona utukufu wa Mungu (mash. 1,5).
7. Mke wa Isaya alizaa mtoto nyuma kidogo, lakini Bwana Yesu Kristo alizaliwa na bikira Maria mia za miaka nyuma.
8. Maana ya jina lake ndiyo hii: Mungu atatuma majeshi ya adui kuondosha hazina za Suria na Israeli (sh.4).
9. Shairi 6.
10. Shairi 12.
11. Wakati Bwana atakaporudi (sh.6).
13. Malaika watakatifu (sh.3), na Wamedi (sh.17).
14. Mfalme wa Babeli alikuwa mfano wa Lusifero au mwana wa asubui (sh.12).
16. Kwa sababu watu wa Moabu walikuwa wenyewe kiburi sana (mash. 6,7).
17. Mashairi 1-3. Baki la sura hii ni juu ya Israeli.
20. Mungu alimwagiza kufanya neno hili kama alama kwa Wamisri (sh.3).
22. Eliakimu (mash. 15,21).
24. Bwana ye ye mwenyewe (sh.23).
26. Ndiyo, lakini watahukumiwa nyuma kidogo (mash. 10,11).
28. Bwana Yesu Kristo (Waroma 9:33).
30. Shairi 21.
32. Mfalme wa haki, ndiye Bwana Yesu Kristo (mash. 1,2).
34. Ziwa la moto pahali waovu watakapoazibiwa kwa milele (Ufunuo 14:7; 19:3).

## MAJIBU

36. Alitaka watu wa Yerusalem kuasi mfalme (mash. 13-15).
37. Saniharibu alikuwa ametukana jina la Mungu na Mungu alijibu maombi ya Isaya aweze kulinda Yerusalem (mash. 21-23).
38. Aliomba Mungu na alifanya neno ambalo Isaya alimwagiza kufanya (mash. 3,21).
39. Alijivuma kwa sababu mfalme mkubwa alikuwa ametuma zawadi kwa yeye (sh.2).
42. Matayo 12:18-21.
43. Taifa la Israeli.
44. Mtu mmoja alifanya sanamu yenyewe na mikono yake, na sanamu hii haikuweza kufanya hata neno moja (mash. 9-20).
45. Wazao wa Daudi waliongoza Waisraeli kufanya zambi, hivi Mungu alitoa Waisraeli kwa Mataifa wawatawale.
46. Sanamu haziwezi kutembea na miguu, lakini Mungu anaweza kubeba watu wake na kuwasaidia.
48. Maana ya jina hili inaonyesha ya kwamba Mungu ni wa milele, lakini yeye ni mwenye haki na neema vilevile.
50. Alifika mbele ya Mungu asubui mapema na Mungu alimfundisha (sh.4).
52. Bwana Yesu Kristo.
53. Wakati wanapompokea kama Zabihu kwa zambi zao (sh.10).
55. Alisema mawazo ya Mungu ni makubwa na juu kupita mawazo yetu (sh.9).
57. Ndani ya shairi 15 anasems ya kwamba ataishi pamoja na watu wanaokiri zambi zao kweli kweli.
60. Shairi 11 na shairi 16 vilevile.
61. Rehemu ya kwanza ya shairi 2 inasema juu ya kuja kwake kwa kwanza kwa neema, na sehemu ya pili inasema ya kwamba atarudi tena kuhukumu dunia.
63. Huu ni mfano wa Bwana Yesu akihukumu adui zake wakati atakapokuja tena.
66. 65:17; 66:22. Soma vilevile 2 Petro 3:13.

**ISAYA**